

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
1 machi 2008**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mohamedi
Aseli Wilison
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Jumanne Idd Selemani
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Paulo Atibu Hatibu
Prosper Andrew Assenga
Sudi Saidi Ramadhan

Ofisi, guta na mambo ya hela

Ally Saidi Mohammed alisema alikuwa na shida kusafirisha ubao wa tangazo ofisini lakini sasa tulimwambia ataweza kutumia guta la UWABA na atashughulika pamoja na Jumanne na kuiweka wiki hii. Tuliongeana kuhusu vipi karatasi zitasimama vizuri kwenye rafu na Ally Saidi Mohammed alipendekeza tutumie kamba na hooks. Tulinunua kamba kwa Tsh 1,000 kutoka machinga na Ally Saidi Mohammed na Juma watafuatilia zitengenezwe wiki hii.

Wakati wa wiki Mejah na Juma walichukua Tsh 60,000 kutoka benki. Walinunua rangi na vifaa vya rangi kwa Tsh 47,000 na walimlipa fundi Tsh 14,000 kupaka rangi ndani na nje ya ofisi kwenye rangi nzuri, na sasa ofisi inapendeza zaidi. Pia walilipa Tsh 2,500 kwa kiasi ndogo ya sementi kujaza mashimo. Mejah alimwambia Elaine atapaka rangi ya jina na nembo za UWABA nje ya ofisi kesho. Tsh 2,000 kutoka hela ya guta ya wiki jana ilitumikwa na Juma anabaki na Tsh 5,000.

Ally Saidi Mwishehe hakuwepo kwenye mkutano na hatujaweza kupokea hela ya guta ya wiki hii.

Tawi la Temeke

Wakati wa wiki Elaine alitengeneza vipeperushi kutangaza mkutano wa kwanza wa tawi la Temeke la UWABA jumamosi ijayo, na Paulo alizisambaza Temeke. Alileta vipeperushi zaidi kwenye mkutano na Paulo na Hussein Hamisi walizichukua kuzisambaza Temeke.

Tulikubali kwamba wanachama wa Mabibo watakutana saa mbili na nusu Mabibo na kuendesha baisikeli pamoja mpaka Temeke. Mkutano Temeke unanaza saa nne. Juma ataleta bendera na Elaine ataleta fomu za wanachama na kamera.

Wamba Memorial Fund

Hatujapata jibu la email kutoka Wamba memorial fund bado. Labda lazimba kumpigia simu mwenyekiti wa fund merekani kuuliza.

ATD Fourth World

Wakati wa wiki Elaine alikutana na watu watatu wa ATD Fourth World, shirika linolosaia watu kwenye hali ngumu, na aliwaambia kuhusu UWABA. Walitualika kuhudhuria mkutano wa shirika lao Maktaba ya Taifa tarehe 15 Machi mchana.

Diwani wa Ilala

Diwani wa Halmashauri ya Ilala ambaye alikuwa mgeni rasmi katika msafara wa baisikeli 2007, Bwana Lupilya, alipigia simu kusema amenunua baisikeli yake na kwa watoto wake na atapenda kushirikiana katika matukio yetu. Elaine alipendekeza tumwalike kwenye ufunguzi rasmi wa ofisi yetu.

Maswala yanayobaki

Juma atafuatilia majibu ya barua zetu Umoja wa Ulaya na Halmashauri ya Jiji wiki hii. Maswala mengine kufuatilia ni kupata watu kushiriki katika mashindano ya kuandika mawazo/hadithi kuhusu baisikeli kwa watoto na kupata mkutano na polisi wa trafiki.